



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA

Barua zote ziandikwe kwa:  
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Simu Na 023 2402738,  
MKURANGA,  
Fax Na 023 402706  
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 10,

PWANI.

Kumb. Na. LD/MK/7120/7

TANZANIA INVESTMENT CENTRE

RECEIVED

6/12/20

21 DEC 2021

P. O. Box 938  
DAR-ES-SALAAM

Mkurugenzi Mkuu,  
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,  
S.L.P.938,  
Dar es salaam

### YAH: KUITAMBULISHA KAMPUNI YA FEDERAL FOOTWEAR INC LIMITED KUNUNUA ENEO LENYE KIWANJA NA.44 KITALU 'F' MWANAMBAYA, WILAYA YA MKURANGA


Rejea mada tajwa hapo juu.

Ninakujulisha kwamba, Kampuni ya **Federal FootWear Inc Limited** ni Kampuni yenye kumilikiwa Raia wa nje ya nchi. Kampuni hii imenunua eneo la Ardhi ambalo wamelipanga na kulipima na sasa linajulikana kama kiwanja Na.44 kitalu F mwanambaya, Wilaya ya Mkuranga kutoka **Kundaeli Hezekiel Lema**.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya inaitambulisha Kampuni hii kutoka nje ya nchi ili iweze kupatiwa Certificate of Incentive kwa kiwanja Na.44 Kitalu 'F' Mwanambaya ili kuwezesha kuandaa **Designation for Investment-Land form Na.1** ili kiwanja hiki kigawiwe katika **kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa** na hatimaye kutangazwa kuwa eneo la Uwekezaji katika Gazeti la Serikali.

Ninaambatanisha ramani ya upimaji, sale Agreement, MoU and Article of Association, hati ya usajili wa Kampuni na uthibitisho wa Uraia wa wamiliki wa Kampuni ili taratibu za kuwasajili zifanyike  
Naomba kuwasilisha kwako kwa hatua zaidi,



Chagiye R.M  
Kny.Mkurugenzi Mtendaji (W),  
**Mkuranga**

**Nakala:** Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**Mkuranga** -Kwa taarifa

Federal FootWear Inc. Limited  
**Dar es salaam** -Fuatilia nyaraka husika TIC